City School District of ALBANY

Mwongozo wa Kifaa Kimoja cha Mafunzo cha Chromebook kwa Mwanafunzi Mmoja

2020-2021

YALIYOMO 2

LENGO LA KIFAA KIMOJA KWA MWANAFUNZI MMOJA 2

WAJIBU 2

WAJIBU WA MWANAFUNZI 2
WAJIBU WA MZAZI 3
WAJIBU WA WILAYA 3

MWONGOZO WA MATUMIZI YENYE UWAJIBIKAJI 3

UTUNZAJI WA JUMLA 3
MATUMIZI & UTUNZAJI WA JUMLA 4

USAIDIZI & UKARABATI 4

USAIDIZI & UTAFUTAJITATUA 4
UKARABATI & GHARAMA 5

MKATABA WA MWANAFUNZI 6

YALIYOMO

Lengo la Kifaa Kimoja kwa Mwanafunzi Mmoja

Lengo la Mpango wa Wilaya ya Shule ya Albany wa kifaa kimoja cha mafunzo cha Chromebook kwa mwanafunzi mmoja (1:1) ni kutoa zana na nyenzo kwa Mwanafunzi wa Karne ya 21. Ufanisi kwenye elimu unahitaji teknolojia ijumuishwe bila kikomo katika mpango mzima wa elimu. Kuongeza ufikiaji wa teknolojia ni muhimu.

Teknolojia ya mafunzo imethibitishwa kukuza kushiriki kwa mwanafunzi na kuongeza shauku ya masomo, huku ikiwasaidia wanafunzi kupata ufahamu na stadi za kufikiria. Lengo la mpango wa kifaa kimoja kwa mwanafunzi mmoja ni kuwa wanafunzi watajifunza, kushiriki, kushirikiana, kuchambua kwa fikra, na kutatua matatizo kwa kujumuisha teknolojia na mbinu bunifu za mafunzo kila mara na kwa uwazi.

Wanafunzi wanatarajiwa kutumia rasilimali za wilaya za teknolojia na mtandao kwa uwajibikaji, huku wakiweka vifaa walivyopewa na wilaya vikiwa salama, thabiti na vikiwa vinaweza kufanya kazi vizuri. Maelezo yaliyo kwenye mwongozo huu yanabainisha wajibu wa kila mhusika na yatawasaidia wanafunzi na wazazi kutimiza mtarajio haya.

WAJIBU

Wajibu wa Mwanafunzi

Tunatarajia na kuamini kuwa wanafunzi watatumia teknolojia kwa kuwajibika na kwamba wanaelewa matumizi yanayofaa na yanayokubalika ya rasilimali za teknolojia na mtandao za Wilaya. Matarajio haya ya Wilaya sio kwa vifaa vya shule zetu tu bali pia kwa vifaa vya mwanafunzi mmoja kuwa na kifaa kimoja (1:1) vinavyopewa wanafunzi na familia kwenda nazo nyumbani. Matumizi ya wanafunzi ya vifaa vya wilaya, nyumbani, yanachukuliwa kwa kiwango sawia na matumizi ya shuleni, na yanafuata sera zifuatazo za Wilaya:

- Matumizi Yanayokubalika ya Mtandao wa Kompyuta na Intaneti (4526, 4526.1, & 4526R)
- Kanuni za Maadili (5300)
- Matumizi Yaliyoidhinishwa ya Nyenzo na Vifaa vya Wilaya (8330)

Kando na sera na taratibu zinazothibiti matumizi na tabia ya wanafunzi, Wilaya inatarajia kuwa:
Wanafunzi **Wata**-

- Tumia hekima katika utunzaji na udumishaji wa teknolojia ya kompyuta inayotolewa na wilaya.
- Rejesha Chromebook waliyopewa mwishoni mwa mwaka wa shule (au mwa usajili wa mwanafunzi) kwa wilaya ikiwa katika hali sawia na vile walivyoipokea.
- Linda kifaa chao nyakati zote.
- Ripoti uharibifu wowote au kuibwa kwa kifaa kwa mwalimu/mzazi/msamamizi wa shule haraka iwezekanavyo.
- Chaji kifaa chao cha 1:1 kila usiku, na kuhakikisha kuwa kiko tayari kutumiwa kila siku kikiwa na chaji ya kutosha. Vifaa vilivyochajiwa kamili huwa na chaji ya kudumu siku nzima ya shule. Nyaya za kuchaji/chaja zinapaswa kuachwa nyumbani.
- Fuata kanuni za mtumiaji wa teknolojia katika matumizi ya vifaa vya Chromebook vinavyopeanwa na wilaya.

Wanafunzi **Hawata**-

- Weka alama, kuharibu, au kuweka vibandiko kwenye kifaa walichopewa na shule.
- Jaribu kupuuza, kuepuka au vinginevyo kubadili programu ya kuchuja Intaneti, mipangilio ya kifaa, maunzi, programu, au usanidi wa mtandao.
- Tumia kifaa walichopewa na Wilaya kwa madhumuni ya kibiashara au kisiasa.
- Sakinisha programu za matumizi ya kibinafsi (michezo, mitandao ya kijamii, kutuma ujumbe, n.k.) na/au za kujinufaisha.

Wajibu wa Mzazi

Kama ilivyo na mafanikio yoyote ya mwanafunzi, wazazi wana jukumu muhimu la kuyaunga mkono. Ni muhimu kwa wazazi kuwajibika kwa kiasi fulani katika mafanikio ya mpango wa kifaa kimoja cha Chromebook kwa mwanafunzi mmoja. Wilaya inatarajia kuwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi anayepewa Chromebook ata:

- Fuatilia kwa ujumla matumizi ya kifaa hicho, hususan kujadili vikomo vya muda na mahudhui ambavyo mtoto wako anapaswa kufuata anapotumia Intaneti au kuona vyanzo vya taarifa vya vyombo vya habari vya kidijitali.
- Hakikisha ndugu na jamaa wengine hawatumii kifaa kwa shughuli za kibinafsi.
- Gharamia utengenezaji au ununuzi wa kifaa kipya ikiwa hakijarudishwa, kimeharibika, kupotea au kuibwa.
    - Ni LAZIMA ripoti ya polisi iwasilishwe iwapo kitaibwa.

Wajibu wa Wilaya

Wilaya ya Shule ya Mji wa Albany inashiriki katika wajibu wa kuhakikisha mpango umefanikiwa kando na kutoa vifaa tu. Ili kukuhakikisha kuna mazingira salama, thabiti na yanayofaa ya kutumia vifaa vya mafunzo, Wilaya ita:

- Toa huduma ya kuchuja Intaneti shuleni na nje ya shule. Kwa sababu hakuna suluhu ya kuchuja maudhui yenye ufanisi wa 100%, ufuatiliaji na utambuzi ni muhimu sana pia.
- Chunguza ufikiaji na matumizi yasiyofaa ya rasilimali.
- Toa sasisho za programu na usalama kiotomatiki, shuleni na nje ya shule.
- Fanya matengenezo ya kimsingi kwa gharama ya chini. Ukarabati mkubwa utahitaji huduma za kitaalamu kwa gharama ya juu.
    - Ni marufuku kwa wanafunzi na wazazi/walezi wao kujaribu ukarabati wowote wa Kifaa chao cha 1:1. Kifaa chochote cha 1:1 kinachokuwa na matatizo au kinachohitaji kukarabatiwa au kutengeneza lazima kirudishwe kwa Wilaya ili kupata usaidizi wa kiufundi na/au kukarabatiwa.

MWONGOZO WA MATUMIZI YENYE UWAJIBIKAJI

Utunzaji wa Jumla

Kutumia busara na utunzaji wa kimsingi kutawezesha kifaa cha Chromebook kutumika kwa miaka mitano (5) bila tatizo lolote. Ni muhimu sana kutekeleza hatua za kimsingi ili kuwezesha kifaa cha Chromebook kuwa katika hali bora zaidi ya kufanya kazi kila wakati.

- Tumia tu kitambaa safi na laini kupangusa skrini, usitumie vifaa vya kusafisha vya aina yoyote.
- Nyaya na kebo lazima ziingizwe kwenye kifaa cha Chromebook vizuri ili kuzuia kuharibika.
- Vifaa vya Chromebook vinaweza kuathiriwa kwa urahisi na joto au baridi nyingi; epuka kuviweka kwenye mazingira kama haya.
- Funga kifuniko kwa upole baada ya kumaliza kutumia Chromebook. Usigonganishe kifuniko cha Chromebook unapoifunga kwa sababu kufanya hivyo

kunaweza kuharibu skrini.
- Usiwahi kuacha vifaa vya Chromebook bila kuwa na mtu karibu kwenye eneo lisilofungwa au bila mwangalizi.
- Vifaa vya Chromebook huenda vikawekwa kwenye kabati ya mwanafunzi huku ikiwa imefungwa kwa kufuli. Hakuna kitu chochote kinapaswa kuwekwa juu ya kifaa cha Chromebook kinapokuwa kwenye kabati.

Matumizi & Utunzaji wa Jumla

Vifaa vinavyopeanwa na wilaya hutolewa ili kutoa uzoefu thabiti wa mafunzo shuleni na nyumbani. Sera zote zilizopo ambazo zilitambuliwa hapo awali zinathibiti matumizi ya vifaa nyakati zote na katika maeneo yote. Kando na sera zinavyovithibiti, vifaa vinavyopeanwa na wilaya vinaweza:

- Kukusanywa na kuchunguzwa wakati wowote: Sababu za kuchunguzwa kwa vifaa vya Chromebook huenda zikajumuisha lakini sio tu zifuatazo: utendaji, udumishaji, uwezo wa kufanyiwa ukarabati, na tabia ya mwanafunzi anapotumia Chromebook.
- Wanafunzi wasitarajie pawepo na usiri au ufaragha katika matumizi yoyote ya Chromebook. Wilaya huenda ikaingia, kusimamia, kufikia, kuangalia, na kufuatilia matumizi ya vifaa vya Chromebook vya wanafunzi wakati wowote, bila notisi au idhini yoyote, kwa sababu yoyote inayohusiana na shughuli za Wilaya.
- Vifaa vyote vya Chromebook vitakuwa na lebo ya mali ya Wilaya. Lebo hiyo ya mali huenda isibadilishwe au kugeuzwa kwa njia yoyote ile. Huenda wanafunzi wakatozwa ada ya gharama ya kifaa kingine cha Chromebook kwa kubadilisha lebo ya mali ya Wilaya au kurudisha kifaa cha Chromebook kisicho na lebo ya mali ya Wilaya.
- Wakati kifaa hicho kinatumika shuleni, kwa kazi za darasani, mwanafunzi anapaswa kutumia kifaa kwa kazi inayohusiana na darasa pekee. Mwanafunzi akipatikana akifanya kitu chochote ambacho hakina uhusiano wa moja kwa moja na darasa, huenda akapoteza haki na hatua inayofaa ya kinidhamu itachukuliwa.
- Vifaa vya Chromebook vina kamera. Wilaya **haina** uwezo wa kufikia kamera hizo kwa umbali. Kamera za vifaa hazitatumika kuwafuatilia wanafunzi.

USAIDIZI & UKARABATI

Usaidizi & Utafutajitatua

Ingawa vifaa vya Chromebook ni rahisi sana kutumia na kutegemea, kuna nyakati zinazohitaji usaidizi. Usaidizi wa jumla wa kiufundi unapatikana wakati wa saa za kawaida za biashara kwa kuwasiliana na Kituo cha Usaidizi wa Kiufundi (518.475.6175). Ni muhimu kukumbuka kuwa Kituo cha Usaidizi kinaweza tu kutoa usaidizi mdogo wa kiufundi unaohusiana na vifaa vinavyopeanwa na wilaya.

Usaidizi wa vifaa vya mtu binafsi haupo. Usaidizi unaohusiana na masomo ya mtandaoni unapaswa kuelekezwa kwa mwalimu au msimamizi wa shule. Wilaya ina nyenzo nyingi za teknolojia ya mafunzo/mafunzo ya mtandaoni zinazopatikana kwenye kiungo hiki kwenye tovuti ya Wilaya:
https://www.albanyschools.org/academics/distance-learning

Fundisanifu atajaribu kusuluhisha matatizo akiwa mbali, kwa njia ya simu, pale iwezekanavyo. Fundisanifu akitambua kuwa kifaa cha mwanafunzi kinahitaji kutengenezwa akiwa nacho karibu, fundisanifu ataunda tiketi na kumwelekeza mwanafunzi kupeleka kifaa chake kwa ofisi ya shule au msimamizi wa Chromebook aliyeteuliwa.

Kabla ya kuwasiliana na Wilaya kwa usaidizi, hatua zifuatazo za kimsingi za utafutajitatua huenda zikasuluhisha tatizo:

- Mwongozo wa utangulizi wa matumizi ya Chromebook unaweza kupatikana kwenye tovuti ya Wilaya katika: https://www.albany.k12.ny.us/portals/0/documents/chromebook_intro_guide.pdf
- Kila wakati jaribu kuwasha kifaa upya kama hatua ya kwanza ya utafutajitatua.
- Ikiwa huwezi kufikia intaneti, hakikisha kuwa muunganisho wa pasi waya umewezeshwa, na kifaa kimeunganishwa kwa mtandao.
- Hakikisha kuwa betri ina chaji. Ikiwa haina, unganisha kifaa kwa nishati ukitumia waya.
- Wanafunzi wanaweza kusimika printa zao za nyumbani kwa kutumia huduma ya Google Cloud Print ili kuchapisha kutoka kwa vifaa vyao vya Chromebook wakiwa nyumbani. Maelezo kuhusu huduma ya Google Cloud Print yanaweza kupatikana hapa: .http://www.google.com/cloudprint/learn/
- Wanafunzi katika gredi za 6-12 wanapaswa kutumia mfumo wa Wilaya wa usimamizi wa nywila wa kujisaidia ili kubadilisha na kuweka upya nywila zao. Mwongozo wa kujisajili na kutumia mfumo huu unaweza kupatikana hapa:
    - Nyenzo ya Kuweka Upya Nywila: https://ssrpm.albany.k12.ny.us
    - Video ya Mafunzo: https://youtu.be/yQM25wmLZ4I

Ukarabati & Gharama

Kwa sababu ya kutekelezwa kwa mpango wa kifaa kimoja kwa mwanafunzi mmoja katikati ya mwaka, thamani ya chaguo ya bima imebatilishwa. Kwa mwaka wa shule wa 2020-2021, wilaya haigharimii mpango wa bima ya mtu binafsi. Kuanzia kupeanwa tena kwa vifaa vya mwaka wa shule wa 2021-2022, kutakuwa na chaguo la bima inayogharimiwa na familia. Maelezo kuhusu ada ya kila mwaka na kinachogharimiwa na bima yatatolewa kuelekea mwanzoni mwa mwaka ujao.

Vikitunzwa ipasavyo na kutumiwa kwa uwajibikaji, vifaa hivi vya kudumu vitahitaji matengenezo au ukarabati mdogo sana au hata havitahitaji wowote. “Bima” inayofaa na ya gharama ya chini zaidi ni umiliki wenye uwajibikaji. Wilaya ya Shule ya Mji wa Albany itagharamia ukarabati wa kifaa kitakachoharibika kutokana na matumizi ya kawaida au kitakachokuwa na dosari ya utendakazi. Gharama za visa vingi kwa mwanafunzi/kifaa kimoja na uharibifu mwingine wowote, kupotea, au kuibwa—iwe ni kwa kukusudia au bila kukusudia— zitakuwa ni wajibu wa mwanafunzi. Hizi hapa chini ni ada za ukarabati wa kawaida wa vifaa vya Chromebook kwa mwaka wa shule wa 2020-2021.

Sio aina zote za ukarabati zimeorodheshwa. Ada zinabadilika kulingana na aina ya ukarabati.

Ada ya Ukarabati/Kununua Kifaa	Ada Kamili	Malipo ya	Malipo ya Pili ya	Malipo Mengine Yote
Uharibifu Mbaya Usiokusudiwa	$ 265	Hakuna Ada	50% ya ada	Ada kamili ya
Wizi (pakiwa na ripoti ya polisi)	$ 265	Hakuna Ada	50% ya ada	Ada kamili ya
Kupotea au Kuharibika kwa Sababu	$265	50% ya ada	Ada kamili ya	Ada kamili ya
Kubadilisha Skrini	$100	Hakuna Ada	50% ya ada	Ada kamili ya
Kubadilisha Betri Kabla ya Muda	$65	Hakuna Ada	50% ya ada	Ada kamili ya
Kubadilisha Kibodi	$50	Hakuna Ada	50% ya ada	Ada kamili ya
Kubadilisha Adapta ya Nishati	$35	Hakuna Ada	50% ya ada	Ada kamili ya

Ni marufuku kwa wanafunzi na wazazi/walezi wao kujaribu ukarabati wowote wa Kifaa

chao cha 1:1. **Wanafunzi hawaruhusiwi kupeleka kompyuta yao kwa kampuni au mhusika wa nje katika hali yoyote ile.** Ukarabati wote, usaidizi wa kiufundi na utafutajitatua utafanywa na Idara ya Teknolojia ya Wilaya ya Shule ya Mji wa Albany.

MKATABA WA MWANAFUNZI

Wilaya ya Shule ya Mji wa Albany inachukulia ufikiaji wa kifaa kimoja cha kompyuta kwa mwanafunzi mmoja kuwa muhimu kwa mpango wa elimu. Kwa kumpa kila mwanafunzi kifaa kimoja cha Chromebook cha kutumia shuleni na nje ya shule, lengo la mafunzo ya mwanafunzi yanayomhusisha, yenye ushirikiano, ya kujielekeza, na yanayomwezesha litatimia bila kujali eneo mwanafunzi yupo. Wanafunzi wanatarajiwa kutumia rasilimali za teknolojia na mtandao za wilaya kwa kuwajibika na wazazi wanatarajiwa kushirikiana na wilaya ya shule katika kuhakikisha mtoto wao anatumia kifaa alichopewa na wilaya kulingana na sera mwongozo wa wilaya. Ulio hapa chini ni mukhtasari wa maazimio yaliyotolewa na wanafunzi na wazazi.

Wanafunzi wanakubali majukumu yafuatayo kabla ya, wakati wa, na baada ya shule haijalishi wako shuleni au nje ya shule.

- Kutumia kifaa kwa njia yenye uwajibikaji na inayozingatia maadili, wakizingatia mwongozo wa matumizi yenye uwajibikaji yaliyoelezwa kwenye Mwongozo wa Kifaa Kimoja cha Mafunzo cha Chromebook kwa Mwanafunzi Mmoja na sera hizi;
    - ❖ Matumizi Yanayokubalika ya Mtandao wa Kompyuta na Intaneti (4526, 4526.1, & 4526R)
    - ❖ Kanuni za Maadili (5300)
    - ❖ Matumizi Yaliyoidhinishwa ya Nyenzo na Vifaa vya Wilaya (8330)
- Kutumia teknolojia kuunga mkono masomo na kazi zinazofaa shuleni.
- Epuka kuharibu kifaa kwa kukitunza na kukilinda.
- Mjulishe mfanyakazi wa shule au mzazi/mlezi mara moja ukiona maelezo, picha, au ujumbe usiofaa, hatari, unaokutisha, au unaokusumbua.
- Linda kifaa nyakati zote.
- Kuja na kifaa cha Chromebook shuleni kikiwa kimechajiwa kikamilifu.
- Rejesha Chromebook mwishoni mwa mwaka wa shule (au mwa usajili wa wilaya) ikiwa katika hali sawia na vile ulivyoipokea. Vifaa haviwezi kutumika baada ya mwanafunzi kuhama kutoka wilaya husika. Kukosa kurejesha kifaa kunaweza kukufanya ushitakiwe kwa kosa la jinai.

Mimi na mtoto wangu tumesoma, tukajadili na kukubali wajibu na matarajio yaliyoelezwa kwenye fomu hii na vilevile kwenye Mwongozo wa Kifaa Kimoja cha Mafunzo cha Chromebook kwa Mwanafunzi Mmoja.

HAKIKISHO LA MWANAFUNZI
Jina la Mwanafunzi (usishikanishe herufi): _____ Utambulisho wa Mwanafunzi: _____
Saini ya Mwanafunzi: _____ Tarehe: _____

HAKIKISHO LA MZAZI
Jina la Mzazi: _____
Saini ya Mzazi:_____ Tarehe: _____